HOTUBA YA MHE. JAKAYA MRISHO KIKWETE, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE UFUNGUZI WA JENGO LA UKUMBI MPYA WA BUNGE, DODOMA , 12 JUNI, 2006

Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri wa Muungano wa Tanzania;
Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein;
Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume;
Waziri Mkuu, Mhe. Edward Lowassa
Mheshimiwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar,
Mhe. Pandu Ameir Kificho;
Waheshimiwa Maspika Waalikwa;
Waheshimiwa Mawaziri;
Waheshimiwa Wabunge;
Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa;
Wageni Waalikwa;
Mabibi na Mabwana.

Niruhusuni niungane nanyi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha salama siku ya leo kutukutanisha pamoja hapa siku ya leo kushuhudia ufunguzi wa Jengo Jipya la Ukumbi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunialika kushiriki kwenye shughuli hii. Mmenipa heshima kubwa kwa kunishirikisha kwenye tukio hili la kihistoria. Nawashukuru kwa mapokezi mazuri.

Naomba pia nitumie fursa hii na mimi kuongeza kauli ya kuwakaribisha wageni wetu kutoka nje ya nchi. Nafurahi kwamba

mmeweza kujumuika nasi, jambo ambalo linaasharia ukaribu na udugu uliopo baina ya nchi zetu na watu wake.

Mheshimiwa Spika,

Mnamo mwezi wa Februari, 2005 tulikuwa hapa, tukiongozwa na Mhe. Frederick Sumaye, Waziri Mkuu wa wakati ule kwa ajili ya kuweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa Jengo hili. Kazi hiyo sasa imekamilika hiyo sasa imekamilika na ushahidi ni jengo hili linalopendeza lililoko mbele yetu na sherehe ya leo.

Nafarijika sana kuungana nanyi leo, takriban miezi kumi na saba baadaye, katika sherehe za ufunguzi wa jengo jipya la Bunge. Sherehe ambayo imefana sana. Kuanzia kesho Waheshimiwa Wabunge mtaanza kulitumia mnapoanza Mkutano wa Bunge la Bajeti. **Hongereni.**

Nawapongeza wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kufanikisha ujenzi wa ukumbi huu. Nawapongeza sana kwa kazi hii kubwa na nzuri. Hususan, napenda kumtambua Spika Mstaafu, Mzee wetu Pius Msekwa kwa kubuni wazo la kuwa na jengo hili na Waziri Mkuu Mstaafu, Mhe. Frederick Sumaye kwa uwezeshaji wa utekelezaji.

Pongezi mahsusi nazitoa kwa Serikali yetu ya Awamu ya Tatu kwa kuridhia wazo la ujenzi wa ukumbi huu na kusimamia maandalizi yote muhimu ya ujenzi wake. Pongezi maalum zimuendee Rais Mstaafu, Mhe. Benjamin Mkapa kwa kukubali wazo

la kujengwa jengo hili na kuafiki utaratibu mzima wa kupata fedha za ujenzi. Uamuzi wake huo ndio uliowezesha kuwepo kwa jengo hili tunalojivunia nalo. Nafurahi kwamba umepata nafasi ya kuja kushuhudia matunda ya kazi yako nzuri.

Napenda pia kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri Mkuu, Mhe. Edward Lowassa kwa uongozi wenu mahiri uliowezesha ujenzi kukamilika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika;

Pongezi na shukrani pia nazitoa kwa Katibu wa Bunge na timu yake, Waziri wa Fedha na Viongozi wengine wa Serikali kwa kushirikiana vyema kwa kushirikiana vyema katika kuhakikisha kazi hii inakamilika kwa ufanisi mkubwa.

Vilevile, shukrani ziende kwa wajenzi wa jengo hili kwa kazi nzuri na kwa Mashirika ya Mifuko ya Pensheni kwa pamoja kukubali kufadhili na kusimamia ujenzi wa ukumbi huu. Mashirika haya ni Public Service Provident Fund (PSPF), Local Authority Provident Fund (LAPF), Parastatals Provident Fund (PPF) na National Social Security Fund (NSSF). Nawapongeza kwa kuwekeza kwenye mradi huu ambao ni fahari na heshima kubwa kwa Taifa.

Sisi katika Serikali tunatambua wajibu wetu wa kuwalipa kwa gharama kubwa mlioingia. Tunawaahidi tutafanya hivyo kama tulivyokubaliana. Mimi na wenzangu Serikalini tunajua kuwa

mmetumia fedha za wanachama wenu ambazo hazina budi walipwe wakati ukifika. Hatutawaangusha.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana

Kujenga ukumbi wa Bunge wenye kukidhi mahitaji ya Bunge letu na hasa kwa mujibu wa mahitaji na mazingira ya karne ya 21 ni changamoto ya aina yake. Lakini, kwa niliyoyaona ndani ya jengo hili changamoto hiyo imejibiwa kwa ukamilifu. Kwa kila hali jengo hili linafanana kabisa na Bunge la wakati tulionao sasa.

Jengo jipya tunalolizindua leo litaliwezesha Bunge letu sasa kuwa na vifaa vipya vya shughuli za kibunge tena vilivyotengenezwa kwa teknolojia ya kisasa. Ukumbi huu utawawezesha Waheshimiwa Wabunge wetu kupata huduma bora na hivyo kufanya shughuli za uwakilishi kwa ufanisi wa kiwango cha juu. Ni ukumbi wenye hadhi ya kimataifa unaowapa Wabunge vionjo vya Bunge katika karne ya 21.

Mheshimiwa Spika;

Kinachonipa faraja zaidi ni kwamba ukumbi huu mpya, tofauti na kumbi zote zilizowahi kutumika kwa shughuli za Bunge huko nyuma, unatoa fursa zaidi kwa wananchi walio wengi zaidi kufuatilia mijadala ya Bunge kwa karibu zaidi.

Kwa kuwezesha ushiriki mpana zaidi wa wananchi kwenye shughuli za Bunge, jengo hili sasa linatuwezesha kupiga hatua kubwa zaidi katika kujenga na kuimarisha demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge

Nilipata kusoma pahala kwamba, wakati jengo la Bunge la Uingereza (The House of Commons) linajengwa upya baada ya kubomolewa wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Winston Churchil alisema "*we shape our buildings, and they shape us*".

Sina shaka akilini mwangu kuwa, kwa hakika jengo hili litabadilisha namna tunavyofanya kazi ikiwa ni pamoja na mienendo na mitazamo yetu kuhusu vikao na maamuzi ya Bunge. Ni matumaini yangu kwamba jengo hili litatubadilisha kwa kutujengea ufahari wa kuwa na mahali pazuri na penye heshima pa kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika,

Kwa ninavyoelewa mimi, jukumu la msingi la Mbunge ni kuyapa sauti matumaini, matarajio, na matakwa ya watu wetu. Wabunge ni vipaza sauti (megaphones) vya Watanzania waliowachagua.

Bila ya shaka kwa kuutumia kwa ukamilifu ukumbi huu wa Bunge ulio mzuri na wenye vifaa vya kisasa, sauti za Watanzania zitasikika bila mikwaruzo. Aidha, matakwa na matarajio yao

yatawasilishwa, kujadiliwa, kufanyiwa kazi na kupatiwa majibu kwa ufanisi zaidi sasa.

Ndugu zangu, leo tumepata Jengo la Bunge jipya, zuri na la kisasa. Tena, ni jengo la kwanza katika historia ya nchi yetu ambalo limejengwa kwa uamuzi wa Bunge na kwa mujibu wa matakwa yake. Bahati nzuri tunalo Bunge lililokomaa kama taasisi na tunao Wabunge waliopevuka kama watetezi halali wa maslahi ya Watanzania waliowachagua. Sasa kazi kwenu.

Vile vile, napata faraja kubwa kwamba tunalo Bunge makini, lenye Wabunge wa mchanganyiko muafaka kwa maana ya vyama, taaluma, fani, jinsia, umri na rika. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge na uongozi wa Bunge kwa juhudi mnazoendelea nazo za kuimarisha taratibu na kanuni mbalimbali za utawala na uendeshaji wa Bunge ili kuongeza ufanisi katika taasisi yetu hii muhimu.

Ni imani yangu kwamba, kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kufanyia kazi, ikiwa ni pamoja na kuwa na mahali penye hadhi na heshima pa kukutania kama hapa, nafasi na mchango wa Wabunge kwa maendeleo ya Taifa letu utakuwa mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika;

Serikali kwa upande wake, itaendelea kuchangia juhudi za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi zenu hapa Bungeni na Majimboni. Tutafanya kila kinachowezekana, kulingana na uwezo

uliopo, kuwapatia mahitaji ya kuwawezesha kuwa Wabunge wazuri kwa wapiga kura wenu.

Hata hivyo, naomba mtuelewe kwamba pale tutakaposhindwa kutimiza yote mnayoyahitaji si kwa sababu ya kupuuza umuhimu wa Bunge bali ni kwa sababu ya kukwazwa na uwezo wa rasilimali. Mahitaji ni mengi, wahitaji ni wengi lakini uwezo una ukomo. Kuwepo kwa jengo hili ni ushahidi tosha kuwa tunajali.

Mheshimiwa Spika;

Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Bunge, kama mhimili huru wa utawala wa nchi yetu. Wote tuna mteja mmoja: Mwananchi wa Tanzania. Ili tumtumikie vizuri na tukidhi matarajio yake, suala la kushirikiana baina yetu halina mbadala na wala halina mjadala. Katu tusifanye kinyume chake. Mimi siamini kwamba ufanisi wa Mbunge unapimwa kwa umahiri wa kupinga hoja za Serikali. Na siamini pia kwamba Serikali makini nayo ni ile ambayo wakati wote inaziba masikio yake kwa maoni na mawazo ya Wabunge. Nawaahidi ushirikiano wangu binafsi na wa wenzangu wote Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Jengo hili, si tu kwamba linapendezesha sura ya Mji wa Dodoma, bali pia linaipa haiba mpya demokrasia yetu. Hiki ni kiota cha mijadala muhimu ya kitaifa, mijadala itakayoamua mwelekeo wa

demokrasia yetu, hatma ya maendeleo yetu na mustakabali wa Taifa letu. Leo tunafungua **ukumbi wa wananchi** kwa kuwa mawazo, maoni na mashauriano juu ya masuala yanayowahusu wao ndimo humu yatakapokuwa yakijadiliwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,

Wakati wa ufunguzi wa jengo jipya la Bunge la Scotland, Oktoba mwaka wa juzi, Edwin Morgan, Mshairi wa Taifa (national poet) wa Scotland aliandika shairi mahsusi, ambalo napenda kunukuu sehemu yake.

"We give you our consent to govern, don't pocket it and ride away.
We give you our deepest dearest wish to govern well, don't say we have no mandate to be so bold.
We give you this great building, don't let your work and hope be other than great when you enter and begin.
So now begin. Open the doors and begin"

Tafsiri:
Tumewapa ridhaa ya kutawala, msiitie mfukoni na kukimbia nayo;
Tunawatakia heri nyingi na mapenzi ya dhati mtawale vyema, msiseme hamkuwa na mamlaka ya kuwa shupavu;
Tunawapa jengo hili kubwa, msiruhusu kazi na matumaini yenu nayo yasiwe makubwa mtakapoingia ndani na kuanza;
Sasa anzeni kazi. Fungueni milango na muanze;

Mheshimiwa Spika;

Ulinialika kuja kufungua rasmi jengo jipya la Bunge letu tukufu. Kwa kukata utepe, nilitimiza wajibu huo. Kwa heshima na taadhima kubwa naomba niseme kuwa sasa Ruksa! Fungueni milango muingie ndani na muanze kazi.

Nawatakia kila la heri.

Ahsanteni kwa kunisikilliza!